
# JamiiYETU

12 WANAFUNZI VYUO VIKUU 'WASILEWE' MIKOPO

14 TAKUKURU MARA INAVYOMULIKA MIANYA YA RUSHWA KATIKA MIRADI



# Hoja watoazo madereva wa malori kutoenda shule

Na Mwandishi Wetu

"TUNAOMBA serikali ione umuhimu na kutamka kuwa, madereva wa muda mrefu wa malori ya masafa marefu yakiwamo yanayovuka mpaka kwenda nje ya nchi hasa waliofanya kazi hiyo kwa muda mrefu; tuseme kuanzia miaka 15 bila kusababisha ajali, wahuishe leseni zao bila masharti magumu."

Katibu wa Chama cha madereva cha Mkombozi Drivers African Group (MDAG), Selemani Mkondo anasema hayo katika mazungumzo na mwandishi wa makala haya alipofika ofisi za gazeti hili, Dar es Salaam hivi karibuni kuzungumzia suala la madereva wa malori wakiwamo wakongwe kulazimika kwenda katika vyuo vya udereva wa malori.

Anasema suala la madereva kuwa na ubora katika taaluma yao ili kuepusha ajali za barabarani zinazogharimu nguvu kazi na rasilimali za taifa kwa kusababisha vifo na uharibifu wa mali ni muhimu.

"Hata hivyo," anasema hilo lifanyike kwa madereva wapya badala ya kuhususisha hata wakongwe waliofanya kazi hiyo kwa muda mrefu bila kusababisha ajali ili hao watambuliwe rasmi na kupongezwa.

"Hawa madereva wamesoma vyuo vya VETA na wakajifunzia kwenye HDV (akimaanisha malori) na kufanya majaribio kwenye mabasi; wakapewa PSV- leseni (leseni za kuendesha magari makubwa ya abiria) yaani walipata leseni za magari hayo yote na kuhakikiwa na polisi, lakini leo wanaambiwa wasome tena," anasema.

Anaongeza: "Hao ndio tunaomba kwa serikali yetu sikivu, waendelee kuhuisha leseni zao bila masharti mengine mbali na yale ya kawaida."

Kwa mujibu wa MDAG, kupungua au kuongezeka kwa ajali si hasa suala la madereva kusoma.

Anasema tafiti na takwimu mbalimbali zinabainisha kuwa, takribani asilimia 70 ya ajali husababishwa na miundombinu kama barabara huku binadamu wakiwamo madereva wakichangia asilimia 30.

Kwa mujibu wa Mkondo, mambo yanayochangia zaidi ajali licha ya uzembe wa baadhi ya madereva ni pamoja na barabara nyembamba, kona nyingi na maporomoko ya mawe kutoka milimani kuelekea barabarani.

"Dereva anapokutana nayo ghafla linakuwa tatizo linalosababisha hata gari kuanguka," anasema.

Anasema ongezeko la ajali za barabarani nchini linachangiwa pia na mishahara midogo waipatayo madereva wakiwamo wa malori ya masafa marefu, hali inayofanya wawe na msongo wa mawazo hata wawapo kazini.

"Hali hiyo inafanya madereva waishi kupitia migongo ya watoto wao ambao wengine hulazimika kuokota chupa za maji, makopo na vyuma chakavu ili wauze na kupata chakula, hali inayochangia utoro kwa wanafunzi shuleni," anasema.

Mkondo anaongeza: "Hali hiyo nayo ina hatari kubwa kwa taifa kwani inashusha elimu na kuchochea uhalifu hasa wizi".

Anasema takwa la madereva hao wote kusoma lina ugumu katika utekelezaji kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni

Inaendelea uk 13

CamScanner